# MBORA WA MANABII

HADHRAT MIRZA TAHIR AHMAD

AHMADIYYA MUSLIM JAMAAT
TANZANIA

**MBORA WA MANABII**

Mwandishi: Hadhrat Mirza Tahir Ahmad -
Khalifatul Masih IV.

© Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania

Chapa ya kwanza: April 2000. Nakala 3000

Kimeenezwa na
Ahmadiyya Muslim Jamaat
P. O. Box 376
Dar us Salaam
Tanzania

Kimechapwa na
Ahmadiyya Printing Press
P. O. Box 376
Simu: 051 - 110473 Fax: 051 - 121744
Dar us Salamm
Tanzania.

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ

Mheshimiwa Meya wa mji wa Hounslow, waheshimiwa Wabunge, na wageni wengine watukufu. Sisi twaichukulia hii kuwa hafla takatifu kwa sababu ya lile jambo litakalozungumzwa hapa. Hii ni heshima kubwa kwangu mimi bali nafurahi sana kuongea nanyi juu ya jambo hili ninalolipenda mno.

Mwanzoni, nimesoma mbele yenu Kalima Shahada. Kisha nikasoma Sura ya kwanza ya Qur'an Tukufu na aya moja ya Sura iitwayo Al-Kahf. Kalima Shahada niliyoisoma ilikuwa ile iliyorefushwa zaidi ya ile Kalima Shahada inayojulikana kwa kawaida. Hii inazo sehemu mbili; ya kwanza; Allah ni Mmoja, hapana Mungu ila Allah; na sehemu nyingine ni Muhammad ni Mtumishi Wake, mja na Mtume. Mkazo ni juu ya kuwa yeye yu mja kabla ya kuendelea mbele kumchukulia kuwa Mtume.

Ile Kalima Shahada fupi ndiyo iliyokuwa machoni pa Bwana Gibbon wakati yeye alipoituhumu. Bwana Bosworth aliandika juu yake kama ifuatavyo:

> Linakaribia sana kuwa pia jambo geni ya kwamba Bwana Gibbon, ambaye kwa jumla kamsema Muhammad kikamilifu, awe aanze kwa kusema, 'Dini ya Muhammad ni ukweli mmoja asilia na uwongo mmoja ulio wa lazima - Yupo Mungu Mmoja na Muhammad ni Mtume Wake.'

Bwana Smith anazidi kuliendeleza jambo hili kwa kusema:

> Haukuwa, jinsi mimi nilivyojaribu kuonyesha, uwongo kwake yeye Muhammad au kwa wafuasi wake; kama ingelikuwa hivyo, dini ya Muhammad isingelikuwa imejitokeza jinsi ilivyofanya, wala kuwa vile ilivyo leo hii.

Twamshukuru Bwana Smith kwa kuhifadhi picha nzuri ya misimamo ya Kimagharibi kuihusu Islam, na hususan kumhusu Mwanzilishi Mtakatifu wa Islam, Mtume Muhammad amani iwe juu yake. Yeye analizungumzia jambo hili sehemu mbili katika historia nami hapa namnukuu:

> Mnamo karne chache za awali za Dini ya Muhammad, Ukristo haukuweza kuthubutu kushutumu wala kuelezea; uliweza tu kutetemeka na kutii. Lakini Waislamu walipokuwa wamepata ushindi wao wa mara ya kwanza katikati ya Ufaransa yale mataifa yaliyokuwa yakiwaogopa, yalirudi nyuma kama kundi la ngo'mbe lifanyavyo wakati mwingine pale yule mbwa mmoja aliyekuwa akiwatimua mbio anaposimamishwa; na ingawaje wao hawakujaribu kupigana, waliweza angalau kuwasingizia wale maadui zao waliokuwa wakitoroka.

Sasa inafuata mifano ya masingizio kama alivyoandika Bwana Smith, yeye anasema:

> Katika visa vya Turpino, vilivyonukuliwa na Bwana Renan, Muhammad mkomeshaji shupavu wa ibada za masanamu, amejigeuza sanamu la dhababu, na, chini ya jina Maumet, yasemekana amekuwa mwabudiwa huko Cadiz.

Kisha anasema:

> Yeye (Muhammad) ndiye Dajjali, mtu wa dhambi, mwenye kijipembe, nami sijui kinginecho minghairi yake; wala sidhani ya kuwa hadi kufikia katikati ya karne ya kumi na nane mwandishi hata mmoja, isipokuwa ajabu ya yule Myahudi Maimonides, anamchukulia (Muhammad) kinyume na kuwa yu mzushi mkubwa na ni nabii bandia.

Ili kuzidi kulipanua jambo hili, yeye anaendelea kusema:

> Visa vya Bafomet, vilivyokuwa vya kawaida katika karne ya kumi na nne na kumi na tano, vinamnasibisha yeye kila kosa, kama Waathanasia walivyomfanyia Arius. 'Yeye ni fasiki, mwizi wa ngamia, Kadinali ambaye baada ya kutofaulu kupata shahada za matamanio ya kila Kadinali, hubuni dini mpya ili kujilipizia kisasi nduguze'.
>
> Hukaa pa wazi 'Motoni'.
>
> Bwana Dante anamtia ndani ya kundi lake la tisa miongoni mwa wapandao mbegu za ugomvi wa kidini.
>
> Kwa upande wa viongozi wa Matengenezo, Muhammad, amani iwe juu yake, mletaji mkubwa zaidi wa matengenezo, hashirikishwi vilivyo, na ile chuki yao dhidi yake, kama lilivyokuwa pengine jambo la kutazamiwa, yaonekana yenye kubadilikabadilika kama ujuzi wao. Lutha haridhiki ya kuwa yeye (Muhammad) si mwovu kuliko Leo; naye Melancthon anamwamini kuwa ndiye Yajuja na Majuja, au pengine hao, yeye ni wote wawili.

Kwa bahati mbaya, ukurasa huu wa kuhuzunisha wenye masingizio na maoni yaliyokithiri ya chuki dhidi ya Mwanzilishi Mtakatifu wa Islam hayakukoma. Hata hivyo twayaona mabadiliko katika upepo ambao umemleta mmoja wa waandishi mashuhuri juu ya Islam toka Uingereza, ambaye ndiye Bwana Carlyle. Yeye alianzisha zama mpya za njia za kuichukulia Islam. Katika zile zama za giza la chuki yeye alikuwa mtu wa huku wa kwanza mwenye ujasiri na utu kutukuza sifa za Mtume Muhammad, amani iwe juu yake, na alikuwa ishara ya kwanza kuashiria ujaji wa majira mapya.

Baada ya Bwana Carlyle mambo yalianza kubadilika, lakini

hayakuishilizia kuwa ni mtindo, badala yake likabakia tu kuwa jambo lililokatizwa. Tunaona ya kwamba katika historia nzima ya kumlaumu Mtume Muhammad, amani iwe juu yake, palikuwepo na wanachuoni waliorejelea misimamo yao ya kale, huku akizaliwa Salman Rushdie hapa na pale. Kuzaliwa kwa mtu kama Salman Rushdie sio jambo geni katika historia ya ukinzani wa kidini; wahusiana sana na ujinga, utovu wa uvumilivu ni kitu anachokijua sana mwanadamu.

Hebu sasa nimgeukie Bwana Carlyle. Katika kitabu chake mashuhuri na kwa baadhi ya watu ni kitabu chake 'kilaumiwa' kwa jina 'Heroes and Hero Worship (yaani Mashujaa na Ibada ya Mashujaa) yeye anasema:

> Lahaula, fikira sampuli hiyo zasikitisha sana ikiwa tutaupata ujuzi wa cho chote katika viumbe halisi wa Mwenyezi Mungu. Hebu tusiziamini kabisa. Zaonyesha upoozaji wa kiroho wa kuhuzunisha sana nazo zilikuwa mauti ya uhai wa roho za watu. Mawazo ya utovu wa Mwenyezi Mungu ulio mkubwa zaidi ya huo mimi nadhani hayajapata kuhubiriwa humu ardhini. Eti ayari alianzisha dini. Kwa nini, ayari hawezi kujenga nyumba ya matofali kama hazizingatii kihalisi asili za saruji, udongo uliochomwa na cho chote kingine anachokifanyia kazi, basi hiyo anayoijenga si nyumba bali ni lundo la takataka. Haitadumu kwa karne kumi na mbili na kukaliwa na (watu) milioni mia moja na thamanini. Itabomoka kwa mara moja.

Kisha anasema:

> Masingizio ambayo juhudi kabambe zimemlundikia mtu huyu yalikuwa yenye kutufedhehesha sisi wenyewe pale tu Bwana Pocock alipomdadisi Bwana Grotious akimwuliza: Li wapi thibitisho la ile hadithi ya njiwa mzoeshwa kudonoa mbaazi sikioni pa Mtume Muhammad na kuonekana kuwa ni malaika. Bwana

> Grotious akimjibu alimtangazia akisema hapakuwa na thibitisho. Huu ndio wakati wenyewe wa kuyatupilia mbali hayo yote.

Kwa maoni yangu, kiini hasa, na kipengele muhimu zaidi katika Kalima ni hili neno Abd, lenye maana ya mja, yule mja mwaminifu kwa Bwana wake kiasi hiki kwamba neno hili pia lina maana ya kuwa mtumishi mtiifu mwaminifu. Leo nimeamua kutoongea juu ya bishara za Mtume Muhammad amani iwe juu yake, lakini nizungumzie utu wake kama mja, akiwa mtumishi tu wa Mwenyezi Mungu na kama mtu mpole aliyepitisha maisha yake yote miongoni mwa nduguze, wafuasi wake na maadui kama mtu mwaminifu.

Kwa minajili hii mimi nimechagua sehemu kadha za maisha yake yenyewe na tutazikariri pamoja nanyi, ili muweze kuamua yeye alikuwa ni mtu wa aina gani.

Mimi nilisema kwamba kuwa Abdu ilikuwa muhimu kwa sababu naamini kwamba kile kipengele cha utume daima kinapingwa. Upande mmoja wa mtume u wazi kumwelekea Mwenyezi Mungu, na kulifanya jambo gumu kwa watu wa kawaida kuamini au kukataa ukweli wake. Huu upande uliozidi sana kutoeleweka hulifanya jambo gumu kwao wao kukipiga picha kimawazo kitu wasichoweza kukishirikia abadan; lakini kama mwanadamu kila mdai (utume) anaweza akaamuliwa vyema tena sawasawa na kila mtu. Ikiwa mtu huyo ni mwaminifu haiwezekani kwake kuwa Mtume bandia.

Nitaanzia na dondoo za wanachuoni wa kimagharibi nami kwa mara nyingine namnukuu Bwana Bosworth Smith:

> Muhammad alikuwa na urefu wa wastani na mwenye mwili madhubuti; kichwa chake kilikuwa kikubwa na juu ya paji lake kubwa la uso, na juu ya miinuko

> myembamba ya nyusi zake palipita mshipa mmoja wa damu, ambao, alipokasirika, uligeuka kuwa mweusi na kuonekana ukipuma. Ilikuwa nadra kwake yeye kukasirika, sina budi kuwaambieni. Macho yake yalikuwa na weusi wa mkaa na makali kwa nuru yake; nywele zake zilijikunja kwa kiasi; na ndevu ndefu, ambazo kama wa-mashariki wengine, alikuwa akizipapasapapasa alipokuwa akitafakari, viliutilia fora uzuri wa sura yake. Mwendo wake ulikuwa wa haraka tena thabiti, 'kama mwenye kushuka toka mlimani'.

Bwana Bosworth anaandika juu ya tabia yake kwa maneno yafuatayo:

> Yeye alikuwa msema machache ..... na mwaminifu. Walimwita 'Al-Amyn', Mwaminifu. Uchungaji wake wa mifugo wa mwajiri wake; safari zake za Syria; labda urafiki wake wa muda mfupi kule na Sergius au Bahira, Mmonaki wa kihistoria; nadhiri yake mashuhuri ya kuwatononesha wadhulumiwa; kuajiriwa kwake na Khadija katika kazi ya biashara, na kufunga ndoa naye baadaye takriban ndiyo matukio pekee ya ki-nje yenye kustahili kukumbukwa katika maisha yake ya hapo mwanzoni.

Akielezea maisha yake ya hapo mwanzoni Bwana Carlyle anatuambia:

> Bali toka mapema maishani yeye alikuwa ametambulikana kuwa mtu mwenye kuwaza sana, wenzake walimwita Al-Amin, mwaminifu, msema kweli tena thabiti, mwaminifu kwa alilosema na alilotenda. Waliona kwamba yeye daima alimaanisha kitu fulani. Kidogo mnyamavu katika maongezi, mnyamavu kabisa

pasipo na la kuzungumziwa lakini msema ilivyo sawa, mwenye hekima, mkweli alipopata kuzungumza, daima akitoa ufafanuzi wa jambo lenyewe. Na hii ndiyo aina ya pekee ya uzungumzaji inayopasa kuzungumzwa. Maisha mazima tunamkuta aliyechukuliwa kwa jumla kuwa mtu thabiti, mkweli, mchukulia mambo kwa dhati, mnyofu na hata hivyo mpole, mkunjufu, mwenye tabia ya kirafiki, mcheshi, hata kushiriki katika kicheko cha wengi. Wako watu ambao kicheko chao si cha kweli kama kisivyokuwa kweli kila kitu kuwahusu wao. Mtu husikia habari za uzuri wa Muhammad, uso wake mzuri, ulioonekana wa busara na uaminifu, rangi yake ya maji ya kunde nyekundunyekundu, macho meusi makali, macho karibu yafanane na ule mshipa wa paji la uso wake uliokuwa ukifura kwa weusi alipokasirika.

Yeye alikuwa ameishi miongoni mwa watu wake kwa muda wa miaka arubaini kabla hajainuliwa na Mwenyezi Mungu kuwa Mtume. Hata wakanushi wakali wa tabia yake hawawezi wakaonyesha doa lolote katika maisha yake hadi kufikia umri ule. Wala hapana kutafautiana au kutopatana miongoni mwa wanahistoria juu ya ukweli huu. Mambo yakiwa hivyo Qur'an Tukufu ikawatambia wale waliomkana kwa kusema.

Hakika mimi nimeishi nanyi maisha yangu yote kabla ya hayo. Kwa nini hamtumii akili zenu. Je, hamwoni ya kwamba mtu aliyeishi miaka arubaini ya maisha yasiyokuwa na dosari kwa ghafla hawezi akageuka kuwa mtukutu wa kupindukia ardhini. Ambaye hakupata kabisa kusema uwongo kuwahusu wanadamu wenzake angelithubutuje kusema uwongo kumhusu Mwumba wake, aliye Mungu aliyempenda sana.

Hadhrat Khadija aliishatajwa hapo mapema kama mwajiri wake. Ndiye aliyekuwa yule bibi tajiri aliyemtuma safari

mbalimbali za kibiashara hadi nchini Syria. Daima alionekana akiwa mwenye kufaulu katika shughuli hizi. Lakini mimi naamini ilikuwepo sehemu moja ya biashara hii ambayo ndiyo iliyofaulu kupita zote, lakini kwa kawaida huwa haitajwi. Bi Khadija mwishowe alipoolewa naye, yeye alikuwa mtu mwenye umri wa miaka ishirini na mitano, ilhali Bi Khadija mwenyewe alikuwa tayari ameisha toka ujanani na kuingia makamoni. Licha ya tofauti hii ya umri, Bi Khadija alipopendekeza posa yake alikubali, na akaishi naye kwa miaka mingine ishirini na mitano. Baada ya ndoa hii kufanyika, huku akimfahamu heshima yake, Bi Khadija alimkabidhi rasilimali yake yote na akampatia kila alichokuwa nacho. Ile biashara niliyoitaja kuwa ya heshima zaidi, yenye shani zaidi na iliyofaulu zaidi, ilikuwa hii. Baada ya kupokea utajiri ule wote wa mali yeye aliwagawia maskini kila kitu, bila ya kujibakizia hata hela moja. Hii pia ni sifa kubwa kwa Bi Khadija, ambaye akiwa mwanamke tajiri zaidi wa Uarabuni, kwa ghafla akawa mmoja wa maskini wake wakubwa, wala hakunung'unika hata kidogo; akiishi mwisho mzima wa maisha yake na Mtume Muhammad amani iwe juu yake, kwa uaminifu mkubwa kabisa. Alimpenda mtu aliyekuwa bado hajaondokea kuwa Mtume. Hata hivyo, haukuwa uzuri wa sura ya mtu yule bali uzuri wake wa kindani, wa kumetameta kama lulu, ndio uliompendeza. Jambo hili lilibainika zama Mwanzilishi Mtakatifu wa Islam alipopokea wahyi wake wa awali toka kwa Mwenyezi Mungu. Yeye alishtushwa sana na nguvu ya wahyi ule hivi kwamba alirudi nyumbani akitetemeka kana kwamba alikaribia kushikwa na homa. Bi Khadija alimdhania yu karibu kuwa mgonjwa na akamfunika blanketi. Baadaye, Mtume Muhammad amani iwe juu yake, akamwelezea kile kisa kilichokuwa kimempata cha malaika kumjia katika sura ya mtu na kumwamuru asome. Alipojihofia yeye mwenywe; huku akiwa ameshtuka nafsi nzima hakuweza kutambua kilichokuwa kikitendeka kwake. Baada ya kusikia habari hii Hadhrat Khadija, r.a., alimjibu akimwambia:

> Mimi nimekujua kwa muda na najua wewe huyashughulikia maslahi ya wanyonge na kuhuzunikia dhiki zao. Wewe u mtu abebaye taabu za wale walioelemewa na uzito wa mateso. Wayarejesha tena maadili yaliyokuwa yametoweka ardhini. Wewe u mpole mwenye huruma kwa jamaa na unauchukulia udugu kwa njia iliyo bora zaidi. Wewe u mkweli na daima umekuwa hivyo. Basi angeliwezaje Mwenyezi Mungu kukuangamiza. Mimi nayaamini hayo uliyonena.

Ulikuwa ni ule usafi wa yule mja wa ndani yake uliomsadikishia mkewe kwamba yeye alikuwa kweli Nabii. katika hali hiyo akawa wa kwanza kumwamini Mwanzilishi Mtakatifu wa Islam na akatambua kwamba haikuwezekana kwa mtu mkweli kuondokea kuwa nabii bandia.

Bwana Bosworth amekielezea kisa hiki kwa maneno yake mwenyewe naye anasema:

> Khadija akamgeukia na akasema:
> Allah hatakufedhehesha. Si wewe umekuwa mwenye kuwapenda nduguzo, mpole kwa jirani zako, mhisani kwa maskini, mtimiza ahadi na mtetea kweli daima.

Kinyume na maoni ya Hadhrat Khadija, r.a., maoni ya marafiki zake wote yaligeuka ghafla baada ya yeye kujitangaza kuwa Mtume toka kwa Mwenyezi Mungu. Wale waliokuwa wakimwita Al-Amin, mwaminifu kupita wote; waliokwenda kwake kuamuliwa ugomvi wao; waliomwamini kabisa na kumfahamu kuwa mtu mnyofu, walianza kumlaumu kwa uwongo wa aina mbaya zaidi. Bwana Bosworth anakariri haya maoni ya watu wa Makka, baada ya tangazo la Nabii Muhammad amani iwe juu yake la kuwa mteule toka kwa Mwenyezi Mungu, kwa maneno yafuatayo:

> Huyoo anakwenda zake mtoto wa Abdullah mwenye uzungumzaji wake wa mbingu. Walimwita mtazama nyota, mshairi mwehu. Babake mdogo alimdhihaki na sehemu iliyokuwa kubwa zaidi ya wenyeji wakampuuza kwa dharau ambayo ni lazima ilikuwa isiyovumilika sana kwake yeye kuliko mateso ya kidhahiri.

Kisha anatuambia kwamba wenyeji wa Makka wakajaribu mbinu za vishawishi na maafikiano, hongo na hata vitisho (inavyotambulikana katika kauli hii ya Mtume Muhammad amani iwe juu yake):

> Wakinikabili na kuliweka jua juu ya mkono wangu wa kuume na mwezi juu ya mkono wangu wa kushoto, na Mungu akiniamuru mimi sitaitangua imani yangu.

Hii siyo kauli au nia ya mzushi, kaandika Bwana Bosworth.

Yeye alikuwa mtu mpole penye kila uhusiano na watu na alikuwa kwa hakika, mnyenyekevu kwake Mwenyezi Mungu. Alikuwa mpole hata kwa wale waliokuwa wamemkubali kuwa yu Nabii wa Mungu. Safari moja huko Madina, baada ya kuwa yeye tayari ameisha kuambiwa na Mwenyezi Mungu kwamba alikuwa Muhuri wa Manabii, hii ikiwa na maana kwamna yeye ndiyealiyekuwa mbora zaidi miongoni mwao, mmoja wa masahaba zake alibishana na bwana mmoja aliyekuwa akimheshimu sana Nabii Yunus, amani iwe juu yake. Yule sahaba wa Mwanzilishi Mtakatifu wa Islam alisema kwamba Nabii Muhammad, amani iwe juu yake alikuwa mbora zaidi, huku yule mwingine akisema kwamba Nabii Yunus amani iwe juu yake ndiye aliyekuwa bora zaidi. Ubishi huu uliporipotiwa kwa Mtukutu Mtume amani iwe juu yake yeye akatamka akisema: "Msinitangaze ubora wangu kuliko Yunus, mwana wa Muta, kwa sababu ni kinyume na heshima za uhusiano wa wanadamu kuendelea kujigambia ubora wa viongozi wenu dhidi

ya viongozi wa wengine. Jambo la ubora wa mmoja kuliko mweingine ni swali la kuamuliwa na Mwenyezi Mungu, sio kitu cha kujivunia. Huo ndio ujumbe tuliopewa, ambao kwa bahati mbaya umesahauliwa na Waislamu wengi hivi leo.

Kisa kama hiki kilifanyika baina ya Myahudi na Mwislamu kuhusu swala la ubora baina ya Nabii Muhammad na Nabii Musa, amani iwe juu yao. Yule Mwislamu akakasirishwa sana na tabia ya ufidhuli ya Myahudi yule na hata akamzaba kibao. Huyu Myahudi akaenda kwa Mtume Mtukufu amani iwe juu yake na akanung'unika. Yule sahaba mhusika akagombezwa sana na Mtume Mtukufu amani iwe juu yake, ambaye alikariri tena maneno yale yale aliyoyatumia katika kile kisa kingine cha hapo mbeleni, akisema: Msinitangulize kuwa bora kuliko Musa. Akaendelea kusimulia mambo bora ya Nabii Musa amani iwe juu yake na akamsifu kwa njia iliyolainisha sononeko za moyo wa yule Myahudi.

Ziko habari za yeye kusimama usiku kucha, akiomba msamaha wa Allah. Masahaba zake waliona kwamba miguu yake ilikuwa ikifura kwa sababu ya muda mrefu wa kusimama katika sala. Hawakuwa wamepata kumwona akitenda dhambi na walimwamini kuwa mtu safi kuliko wote ardhini. Hili liliwashangaza. Wakamwuliza: kwa nini Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, kuomba msamaha kwa Allah. Akawajibu akisema: je, nisimshukuru Mungu wangu kwa fadhili zote alizonijaalia. Safari nyingine wakati swala hili hili la msamaha na uchaji Mungu wa mtu lilipokuwa likijadiliwa, Mtume Mtukufu amani iwe juu yake, aliwaambia masahaba zake ya kwamba hapana mtu ardhini atakaye samehewa kwa sababu ya vitendo vyake vizuri. Ni rehema ya Allah ambayo mwishowe huokoa kutoka nira ya madhambi na ndiyo itakayosababisha uingiaji wa peponi. Maelezo haya yaliwashangaza na mmoja wao akauliza akisema: Ewe Mtume wa Mungu, wewe

hutasamehewa kwa ucha-Mungu wako na vitendo vyako vizuri? La, hata mimi. Nitasamehewa tu kwa rehema ya Mwenyezi Mungu. Kila kitu ni chake, hapana kilicho chetu. Cho chote kile alichotujaalia, tunakitumia na kukitumikisha kadri ya ujuzi wetu na uwezo wetu. Hata mtu mnyofu, aliyepitisha maisha yake yote akitenda vitendo vizuri, hatasamehewa kwa sababu ya vitendo vyake. Vile fursa nzuri nzuri alizopewa na Mwenyezi Mungu.

Tabia yake ya kutotaka makuu haikuwa na mipaka. Alipokuwa akiketi na wafuasi wake, akivaa nguo za kawaida, akila chakula kile kile walichokuwa wakila, yeye hakuketi mahali maalumu. Mara nyingi walipata kukosea ni nani aliyekuwa Mwanzilishi Mtakatifu wa Islam, amani iwe juu yake. Hadhrat Abu Bakar, Mungu awe radhi naye, baadaye alikuja kuwa Khalifa wa Kwanza wa Islam, alikuwa mzee kumshinda na huenda alikuwa na ndevu ndefu zaidi, sina hakika, haya ni makisio yangu tu, lakini kitu fulani umboni mwake kiliwafanya baadhi ya wageni wamwite Mtume wa Mungu. Naye kwa njia ya staha alikuwa akimgeukia Mtume Mtukufu, amani iwe juu yake, na kuwaongoza kwake.

Safari moja Hadhrat Umar, r.a., aliyekuja kuwa Khalifa wa Pili wa Islam, aliomba ruhusa aende akatimize ibada ya Umra; hii ni ziara fupi mjini Makka sawa na Haji. Mtume Mtukufu wa Islam amani iwe juu yake alimtazama na akatamka akisema: Naam nenda, kaitimize ibada ya Umra na tafadhali usinisahau katika maombi yako. Hii ndiyo iliyokuwa hali ya kutojitakia makuu ya yule mtu, ambaye maombi yake aliyategemea kila Mwislamu, hivi kwamba alikuwa akimtafadhalisha mmoja wa watumishi wake amkumbuke katika maombi yake.

Maisha yake mazima alishiriki katika kila aina ya dhiki zilizowakabili Waislamu kwa jumla. Katika Vita vya Handaki anafahamika kuwa aliyedhikika kwa njaa pamoja na wengine.

Zilipogawanywa sehemu za kulichimba handaki lenyewe, yeye hakuachwa kando na akachangia fungu lake kuchapa kazi. safari moja sahaba mmoja alimwona Mtume Mtukufu, amani iwe juu yake katika hali isiyovumilika. Akasema sahaba huyu: Siku ya vita vya Handaki, nilimwona Mtume Mtukufu akisomba udongo uliokuwa umeufunikiza weupe wa tumbo lake. Alikuwa akisema: Bila ya wewe Ee Mola wangu tusingeliweza kupata mwongozo, wala kutoa sadaka, wala kuomba; tafadhali tumiminie utulivu na uiimarishe miguu yetu tutakapomkabili adui. Hakika watu wametudhulumu lakini kamwe hatukukata tamaa ikiwa watajaribu kututesa kwa sababu yako Wewe.

Hadhrat Jabir r.a., anasimulia kwamba walikuwa wakichimba siku za Vita vya Handaki na wakakuta jiwe kubwa. Wakamripotia Mtume Mtukufu amani iwe juu yake. Alipoinuka wakaona jiwe limefungwa juu ya tumbo lake; alikuwa hajakula cho chote kwa muda wa siku tatu. Ni desturi ya Kiarabu kufunga jiwe namna hii unapoteseka kwa njaa ya kukithiri, huenda hayo yalipunguza ukali wa njaa. Katika hadithi nyingine ya kisa hicho hicho, twakuta kwamba kila sahaba wa Mtume Mtukufu alifungia jiwe juu ya tumbo lake, lakini shati la Mtume Mtukufu lilipoinuka, wakaona tumbo lake limefungiwa mawe mawili. Alipomwona katika hali hii Hadhrat Jabir hakuweza kuivumilia tena. Akamwomba ruhusa na kwenda eneo la akina mama, akamwita mkewe na kumwuliza kama alikuwa na chochote cha kutabaruku. Yule mama akamjibu ya kwamba nyumbani alikuwemo mbuzi na unga pia. Hapo Hadhrat Jabir r.a., akamwambia mkewe amchinje yule mbuzi kwani alikuwa amwemwona Mtume Mtukufu katika hali isiyovumilika asilani.

Huyo ndiye aliyekuwa yule mtu, Nabii Muhammad, amani iwe juu yake, ambaye daima alipata taabu pamoja na watumishi wake. Hapakuwepo na tafauti yoyote ile. Kinyume chake, toka hadithi nyingi juu ya jambo hili tunaweza tukaamini kwamba

yeye aliteseka zaidi.

Alikuwa ni mtu asiyetishika, bila woga ambaye hakusita kuikabili hatari ana kwa ana. Katika maisha yake alipigana vita vingi vya kujihami, ingawaje yeye hakupata hata mara moja kuanzisha vita vya uchokozi. Kwa kawaida yeye alionekana katika zile sehemu hatari zaidi vitani, ambapo mapigano yangeliwaka kama moto. Yaripotiwa na msimuliaji mmoja ya kwamba Mtume Mtukufu alipotakikana katika uwanja wa vita, basi wao wangelimtafuta katika lile eneo la vita ambapo mapambano yalipamba moto zaidi na yeye daima angelikuwa katikati yake. Safari moja mjini Madina, ule mji aliohamia baada ya miaka kumi na mitatu ya mateso mjini Makka, usiku wa manane watu walisikia vishindo vya kugutusha. Katika siku zile yalihofiwa mashambulio toka pande zote, kwa hivyo watu waliwaandaa farasi wao na wakaenda kupeleleza. Badala yake wakamkuta Mtume Mtukufu amani iwe juu yake toka upande ule akiwa juu ya farasi asokuwa na tandiko. Yeye alikuwa ameenda peke yake, kwa haraka, hata bila ya kumtandika farasi wake. Akawaambia haikuweko hatari nao wanaweza wakarudi kwao majumbani.

Siku moja alipokuwa safarini, ikiwa siku ya joto kali, alikuwa akijipumzisha chini ya kivuli cha mti. Bedui mmoja, aliyetokana na waabuduo masanamu, akajionea nafasi yake kwa vile Mtume Mtukufu kajitenga peke yake. Basi akaushika upanga wa Mtume Mtukufu amani iwe juu yake, na akamwamsha huku akimkejeli akimwabia: Nani atakaye kuokoa mikononi mwangu Ewe Mtume wa Mungu. Mtume Mtukufu akajibu Mungu wangu. Hili jibu fupi likamtisha huyu mtu kiasi hiki kwamba mikono yake ikatetemeka na upanga ukajidondokea chini. Sasa Mtume Mtukufu akauchukua ule upanga na kamwuliza yule mtu akimwambia: Ni nani atakaye kuokoa nami? Kwa ghafla mambo yakiwa yamegeuka, mtu huyu aliweza tu kusema kwamba ni

jinsi gani Mtukufu Mtume Muhammad amani iwe juu yake, alivyokuwa mtu mpole na mrehemevu na akamwomba nusra ya maisha yake. Mtume Mtukufu akatamka akisema: Ole wako, hata hukujifunza somo; alikuwa ni Mungu aliyeniokoa dhidi yako. Mtu huyu alisamehewa kwa hakika. Mtume Mtukufu alikuwa mtu mwenye moyo wa huruma sana.

Siku hizi misikiti imekuwa mwahali mwa mikwaruzano duniani kote. Mapenzi juu ya misikiti moyoni mwa Mtume Mtukufu amani iwe juu yake, yalikuwa yamefurika kiasi hiki kwamba ni jambo lisilofikirika kwa mtu mwingine yeyote kuupenda msikiti kiasi hicho. Safari moja Bedui mmoja asokuwa Mwislamu alikuja kutembea Madina na akapatiwa malazi msikitini. Siku zile na hata leo hii katika baadhi ya sehemu za dunia, misikiti yatumiwa kama nyumba za wageni. Pakiwa mahali pa ibada misikiti huwekwa katika hali ya usafi, hata viatu haviruhusiwi ndani. Lakini mtu huyu, kwa sababu ya kutojua, alianza kutabawali mahali pale pale watu waliposali na kusujudu. Na haja hii ndogo ilifanyika akiwepo Mtume Mtukufu na masahaba zake. Baadhi ya masahaba zake wakamhamakia kutaka kumpiga mtu huyu mwenye kuudhi lakini wakakatazwa mara moja na Mtume Mtukufu. walinasihiwa wasimghasi wakati anapojisaidia, Alipomaliza haja yake Mtume Mtukufu akaitisha ndoo ya maji na yeye mwenyewe akapasafisha mahali pale. Kisha akawageukia masahaba zake na akawaambia: Ninyi hamkuinuliwa na Mungu kuwapatia watu shida. Daima kumbukeni ya kwamba mlienuliwa kuwaletea wanadamu faraja.

Safari moja ujumbe mmoja wa Wakristo kutokea eneo la Najran ulifika mjini Madina kwa mjadala wa mada za tofauti baina ya Islam na Ukristo. Wakakaa Madina siku tatu. Walipokuwa wakijadiliana ndani ya msikiti wa Mtume Mtukufu, wakati wa sala yao ukafika. Wakamwomba Mtume Mtukufu ruhusa waende zao nje kwa minajili ya kusali sala yao. Mtume

Mtukufu amani iwe juu yake akasema kwamba msikiti ulikuwa pia mahali pa ibada, na wanakaribishwa kusali mle, nao wakasali mle msikitini. Muda si muda wakafika msikitini baadhi ya masahaba na wakawaona wale Wakristo wakiabudu wakielekea mashariki; tofauti kabisa na wanakoelekea Waislamu katika sala zao. Wakasogea mbele kupinga jambo hili, lakini yeye kwa uthabiti akawakataza wasiwabughudhi Wakristo wale na akatamka akisema: Mimi nimewaruhusu kwa sababu hii ni nyumba ya Mungu, na hapana mwenye haki ya kumkataza yeyote yule mwenye kumwabudu Mungu katika mahali palipo wakfu kwa minajili ya ibada.

Safari moja ujumbe toka makao ya watawa wa Kikristo ya St. Catherine waliandika tangazo lililosema kwamba makao yao yapatiwe ulinzi wakati Islam itakapopata ushindi katika sehemu zile za dunia. Mtume Mtukufu mara moja akalikubali ombi lao na akaandika amri za kulitekeleza. Nifahamuvyo mimi ni kwamba amri hizi bado zinahifadhiwa nchini Uturuki. Amri zenyewe zinasema hivi: Haimpasi yeyote kuingilia rasilimali za Makao ya watawa, wala sanamu ya msalaba au kitu chochote kinachowakilisha dini yao. Na visidhuriwe kwa njia yoyote iwayo. Yeyote atakayelipuuza jambo hili hatakuwa mmoja wetu.

Mengi yanasemwa juu ya chuki iliyopo baina ya Waislamu na Wayahudi. Ingawaje yale makabila ya Wayahudi mjini Madina na pembezoni mwake yalimpinga vikali Nabii Muhammad, moyo wake kumhusu Myahudi kamwe haukuathirika. Safari moja alikuwa ameketi na masahaba zake wakati yalipopitia karibu yao maandamano ya mazishi, akasimama kutoa heshima zake, Mtu mmoja akatamka akisema kwamba maiti yenyewe ilikuwa ya Myahudi. Mtume Mtukufu akajibu: Je, mtu huyu hakupewa uhai na Mwenyezi Mungu? Je, yeye hakuwa kiumbe cha Mungu? Kumbukeni, katika yale mambo yaliyo ya kawaida kwa mwanadamu, ni sharti tuonyeshe

heshima, bila kujali dini ya mtu, taifa au imani. Huu ndio ujumbe wa Islam, haukufundishwa tu wakati wa Mtume Mtukufu bali ulitimizwa kwa dhati katika kila jiha.

Yeye alikuwa mtu mwenye mapenzi yaliyochanganyikana kimaridadi na upole. Aliwapenda watoto, hata aliwaheshimu. Baada ya Mtume Mtukufu kufariki, mmoja wa masahaba zake safari moja alipita kati ya kundi la watoto na akawaamkia Assalaamu Alaikum yaani amani iwe juu yenu. Wao walikuwa bado chipukizi na walishangaa kwamba mzee mwenye kuheshimiwa sana, tena sahaba wa Mwanzilishi Mtakatifu wa Islam aliwatangulia katika kuwatolea maamkizi ya Kiislamu. Yeye akawaambia ni kwa nini alifanya hivyo na akasema: Mimi daima nilimwona Mwanzilishi Mtakatifu akifanya hivyo hivyo, yalikuwa ni mazoea yake kuwa wa kwanza kusema Assalaamu Alaikum, hata kwa watoto.

Hadhrat Anas Osama bin Zaid, Mungu awe radhi naye, anasimulia ya kwamba alipokuwa mtoto, aliinuliwa na Mtume Mtukufu na akakalishwa juu ya goti lake moja, kisha Mtume Mtukufu akamkalisha mjukuu wake Hassan juu ya goti lake jingine, na huku akiwakumbatia wote wawili akimwambia Mwenyezi Mungu: Ewe Mola wangu kawaonyeshe huruma jinsi ninavyowaonyesha huruma. Kisa hiki kilimpatia athari isiyofutika Hadhrat Osama bin Zaid aliyekiripoti huku machozi yakimlengalenga.

Mwanzilishi Mtakatifu wa Islam alikuwa na ucheshi wenye kupendeza sana. Alizoea kuwatania watoto ili kuwachekesha kwa njia rahisi. Lakini utani wake haungelimuudhi yeyote. Tunazo ripoti nyingi za utani wake kwa watoto na wakati mwingine kwa watu wazima pia. Safari moja mama mmoja mzee alimtafadhalisha ya kwamba aombe kwa minajili ya kusamehewa kwake na Allah. Katika kumjibu kwake Mtume

Mtukufu akasema kwamba hapana mtu mzee atakayeingia Peponi. Bila shaka yule mama alishtuka aliposikia hayo. Lakini Mtume Mtukufu alitabasamu na akatamka akisema kwamba yeyote yule aingiaye Peponi hufanywa kijana. Uchekeshaji wake ulikuwa wa hekima na wa kupendeza, ambao daima ulitumiwa juu ya msingi wa mapenzi; wala si kwa nia ya kudharau.

Yeye alikuwa mshikilia uadilifu halisi tena mtimilifu. Hata hivyo nafsini mwake tunaiona sifa hii yake ikienda samabamba na majaaliwa yake ya kuwa na huruma halisi. Katika vita vya Badr ambapo makafiri walienda kuivamia Madina, ami yake mmoja alipokuwa akipigana upande wa makafiri, alitiwa mbaroni na Waislamu. Sawa na mahabusu wengine mikono na miguu yake vilifungiwa kwenye nguzo msikitini. Katika siku zile hazikuwako jela, kwa hivyo misikiti ikatumiwa badala yake. Ikatokea kwamba mtu fulani alikuwa amewakaza kamba mahabusu hawa kwa nguvu sana. Mtume Mtukufu, ambaye maskani yake yalikaribiana na msikiti, hakuweza kupata usingizi usiku ule. Yasemekana kwamba hakupata utulivu na akawa mwenye kugeukageuka ubavu huu na ule kitandani mwake. Masahaba zake wakagunduwa na wakamuuliza ni nini kilichokuwa kikimuhangaisha. Akawajibu akiwaambia kwamba alikuwa akimsikia ami yake akilia huko msikitini. Hapo mtu mmoja akaenda kuzilegeza zile kamba alizofungiwa Bwana Abbas. Baada ya muda Mtume Mtukufu hakusikia tena kwikwi zozote, akapata wasiwasi na akadadisi akisema mbona kwikwi zimeisha. Mtu mmoja akajibu kwamba kamba zake Bwana Abbas zilikuwa zimelegezwa. Mtume. Mtukufu akasema; Kama mmemfanyia hivyo Abbas basi mfanyieni vivyo hivyo kila mahabusu. Hivi ndivyo uadilifu wake ulivyoongezea huruma yake.

Safari moja binti wa chifu mmoja Mwarabu mashuhuri alishikwa akiiba, alikuwa akiitwa Fatima, kama vile bintiye

Mtume Mtukufu. Jambo hili lilikuwa likibishaniwa nje ya nyumba ya Mtume Mtukufu na baadhi ya watu walitaka ahurumiwe kwa vile yeye alikuwa bintiye chifu mwenye uwezo sana. Wakambembeleza Hadhrat Osama bin Zaid. r.a., aliyekuwa mwana wa mtumwa wa zamani wa Mtume Mtukufu, aende akaombe msamaha kwa niaba yake. Kijana huyu alikuwa bado hajaifahamu vyema tabia ya Mtume Mtukufu na akaenda kumwombea msichana yule msamaha. Hili lilikuwa mojawapo ya yale matukio ya nadra ambapo ule mshipa wa paji la uso wa Mtume Mtukufu ulikuwa mweusi, akasema: una maana gani kwa kumtakia msamha. Mimi bila shaka ningelifanya vile Mwenyezi Mungu anitakavyo nifanye hata kama angelikuwa binti yangu Fatima aliyefanya uhalifu huu.

Mtume Mtukufu wakati mmoja alikuwa na pesa za Myahudi. Yule Myahudi akafikiria kwamba wakati wa kulipwa pesa zile ulikuwa tayari umeishapita, kumbe ulikuwa bado haujapita. Akamwendea Mtume Mtukufu na kumdai pesa zake akitumia lugha mbaya sana, na akalaumu akisema kwamba watu wa kabila la Quraishi wote walikuwa kundi moja la wasoio kopesheka ambao kamwe hawatimizi ahadi zao. Hadhrat Umar r.a., ambaye pia alikuwepo pale alikasirika sana  na akataka kumchoma upanga wake. Mtume Mtukufu, akamzuia Hadhrat Umar ambaye sasa alikuwa ameisha  msema mabaya yule Myahudi na pengine alikuwa karibu kumchapa kofi, na akasema; Ewe Umar, ungelitenda tofauti na hivyo. Kwanza ungeliniambia nilikumbuke deni na nilipe wakati wake, kisha ungelimwambia awe na huruma anapodai mali yake na awahurumie wadeni wake. Kisha Mtume Mtukufu akamgeukia sahaba wake mwingine na akasema: Bado zimesalia siku tatu, mimi najua hatujakiuka siku ya miadi, lakini wewe mlipe chochote  anachodai na umpatie nyongeza  kwa sababu ya ukali wa Umar. Hii ndiyo iliyokuwa tabia yake baada ya yeye kutusiwa kidhahiri mbele ya masahaba zake. Uadilifu wake ulikuwa wa kileleni. Ulikuwa uadilifu wa

kupindukia, usiofungamana kwa vyovyote vile na uaminifu wake, kabila au dini yake.

Leo hii uhusiano wa Wayahudi na Waislamu ni kitu kinachoeleweka visivyo na ipo haja ya kukisahihisha. Mimi nitakariri baadhi ya mifano toka kwa uhusiano wa Mtume Mtukufu na Wayahudi kwani ni sharti tuige desturi yake katika uwanja huu; msimamo wowote unaokwenda kinyume hauna budi kukataliwa mbali. Mtume Mtukufu wa Islam amani iwe juu yake alikuwa amejenga picha katika umma ya kuwa mtu mwadilifu kabisa. Hata kama ilikuwapo mikwaruzano baina ya Waislamu na Wayahudi au baina ya Waislamu na waabuduo masanamu, wangelitafuta uamuzi wake. Katika kesi moja inaripotiwa kwamba kipande kimoja cha ardhi kilikuwa kikibishaniwa na Mwislamu na Myahudi. Wao wakamwendea Mtume Mtukufu na kumtaka hukumu yake. Mtume Mtukufu kwanza akamtaka mlalamishi Mwislamu atoe dalili zake. Yule Mwislamu akasema kwamba yeye hakuwa na mashahidi, lakini alikuwa akisema kweli sawa na ahadi. Mtume Mtukufu hakumjali na akamwambia yule Myahudi aape kwa jina la Mungu ikiwa kweli ardhi ile ilikuwa yake. Yule Mwislamu akapinga na akasema: Ewe Mtume wa Mungu, huyu ataapa kiuwongo. Si jambo kubwa kwake yeye kudanganya kwa sababu ya kipande cha ardhi. Mtume Mtukufu akajibu akisema: Hapana njia nyingine ya kuamulia jambo hili, kama yeye ataapa basi ardhi itakuwa yake. Na hivyo ndivyo ilivyokuwa.

Safari moja msafara mmoja mdogo ulitembelea eneo la Khaibar palipokuwa mahali penye kukaliwa na kabila moja la Wayahudi kwa jina la Bani-Nazir. Watu hawa mbeleni walifukuzwa toka Madina na sasa walikuwa wamelifanya eneo hili kuwa makao yao; lakini hiyo ni habari nyingine. Eneo hili sasa lilikuwa ngome ya Wayahudi na tokea hapo lilikuwa likikaliwa nao peke yao. Ule msafara wa kibiashara toka

miongoni mwa Waislamu ulipozuru Khaibar, mfanya biashara mmoja wao aliuliwa. Wakamwendea Mtume Mtukufu na wakapendekeza kwamba kosa la mauaji yale liwekwe juu ya Wayahudi wa eneo lile, na wote kwa pamoja wadaiwe fidia. Mtume Mtukufu akasema: Je, mnao ushahidi wowote wa huyu mtu kuuawa na Myahudi. Wakajibu wakisema: Hapana shahidi lakini ni sharti muuaji awe mmoja wao; hapana mtu mwingine aishiye kule. Mtume Mtukufu akasema: Njia ya pekee iliyopo ni kwamba Wayahudi wale ni sharti waape kwamba hawakufanya mauaji haya. Wayahudi wakafanya hivyo na wakaondolewa hatia ya mauaji yale. Lakini hata hivyo, kwa amri ya Mtume Mtukufu, jamaa wa marehemu aliyeuawa walilipwa fidia toka hazina ya serikali. Katika dhati yake twaona huruma ikiambatana na uadilifu wake kwa njia ya kuvutia na yenye kuafiki zaidi, ambayo kusema kweli inakuwa furaha kubwa kujitazamia.

Yeye pia alikuwa mwenye huruma kwa watumishi wake na watumwa wake. Swala la utumwa ni wazo linaloeleweka vibaya sana upande huu wa magharibi. Mimi sitalifanyia swala hili ufafanuzi wowote, lakini ninawahakikishieni ya kwamba tunayo njia moja tu halali inayotajwa katika Qur'an Tukufu, ambayo kwayo watumwa wanaweza wakahodhiwa. Hii imo katika sura Al-Anfal, aya ya sitini na nane. Aya hii yasema kwamba njia ya pekee ya kuwafanya wanadamu kuwa watumwa ni katika vita vikali mno, sio eti katika mashambulio ya hapa na pale. Katika siku zile haukuwepo utaratibu wa kambi za wafungwa wa kivita, kwa hivyo mateka wa vita wangeligawiwa nyumba mbalimbali. Pia twaona ya kwamba Qur'an Tukufu yapendekeza njia nyingi za kupata uhuru kwa minajili ya wafungwa wa kivita. Zipo aya nyingi juu ya jambo hili, hivi kwamba baada ya kuzisoma, yashangaza ungeliwezaje utumwa kuja kuchukuliwa na Waislam wa leo kama jambo linalohalalishwa na Qur'an Tukufu. Zipo njia nyingi za kujipatia uhuru kiasi hiki kwamba sawa na

Qur'an Tukufu na sunna ya Mwanzilishi Mtakatifu wa Islam, s.a.w., endapo mfungwa wa kivita hakombolewi kwa fidia ya kulipwa na nduguze, na hana njia nyingine ya kujipatia uhuru, anaweza akaenda katika mahakama ya Kiislamu na kutaka aachiliwe mara moja, kwa hili sharti ya kwamba atajichumia kipato kulipia kidogo kidogo bei yoyote inayochukuliwa kuwa ndiyo thamani ya ukombozi wake. Amri hizi za Qur'an Tukufu zilifuatwa kwa dhati wakati Mtume Mtukufu. Wakati mwingine maelfu ya wafungwa yalikombolewa kwa siku moja. Kwa sababu ya yale yaliyotendeka siku zilizopita na pia kwa kuwa hizo zilikuwa nyakati za taabu, badhi ya watumwa walirithiwa na watu na wakaendelea kutumika majumbani. Mtume Mtukufu mara kwa mara aliwanasihi Waislam kwamba wawahurumie chambileche ndugu zao wa damu. Tunakuta vikihadithiwa visa vingi vya aina hii; kwa mfano, wakati bwana na mtumwa wake walipokwenda kununua vitu, mwenye duka hakuweza kuwatafautisha. Safari moja Hadhrat Ali r.a. aliyekuwa Khalifa wa Nne wa Islam baada ya Mtume Mtukufu, alikwenda dukani na akaitisha mavazi mawili yaliyofanana. Mwenye duka akampendekezea anunue mavazi ya rangi zinazotafautiana. Yeye akajibu akisema: Bwana wangu ameniambia niwatendee watumwa wangu kama ndugu zangu wa damu. Hivyo basi, chochote ninachovaa, nitamvalisha hicho hicho mtumwa wangu.

Hadhrat Abu Masud Badri r.a. anasimulia akisema kwamba: Nilikuwa nikimjadili mtumwa niliposikia sauti nyuma yangu ikiniambia: Jihadhari ewe Abu Masud. Nilikuwa nimekasirika hivi kwamba sikutambua sauti yenyewe hadi msemaji aliponikaribia na nikagundua kumbe alikuwa Mtume Mtukufu na alikuwa akisema: Jihadhari ewe Abu Masud, Allah ana uwezo juu yako kuliko ulio nao juu ya mtumwa huyu; nami nikajibu nikisema: ewe Mtume wa Allah, mimi namwachilia huru nipate radhi ya Allah. Mtume Mtukufu akasema: Kama usingelifanya hivyo basi ungelikugusa moto (wa Jahannamu).

Hadhrat Zaid, r.a. hutajwa mara nyingi katika historia ya Islam kwa sababu yeye ndiye aliyekuwa mtumwa pekee kupata kuishi na Mwanzilishi Mtakatifu wa Islam. Anasimulia akisema: Nilipokuwa nikimtumikia Mtume Mtukufu, mimi nilifanya makosa mengi, lakini yeye hakupata kunikaripia, hata mara moja. Hakupata kunilaumu, achilia mbali swala la kunipiga.Wakati wa zama za Madina, baba na ami ya Hadhrat Zaid walipata habari kwamba yeye alikuwa mtumishi wa Mwanzilishi Mtakatifu wa Islam. Basi wakafika mjini Madina na wakamsihi Mtume Mtukufu kwamba amwachilie huru. Akawajibu akisema: Bila shaka mimi nitafanya hivyo lakini kwa nini hamumuulizi yeye? Ni mtu huru. Kama anataka kukaa hapa mimi siwezi nikamshurutisha aondoke. Hapo Mtume Mtukufu akajinyamazia wakati Hadhrat Zaid alipoletwa mbele za baba yake na ami yake. Ukawa mkutano wa machozi ya furaha kwani walikuwa wakikutana baada ya muda mrefu. Wakamtaka Hadhrat Zaid arudi kwao. Yeye akawajibu akiwaambia: Kama chaguo ni langu, basi mimi sitarejea nyumbani kwetu kwa sababu nimegundua mtu ninayempenda zaidi ya baba yangu, mama yangu, ami yangu na mtu mwinginewe humu ulimwenguni. Kusikia hivyo Mwanzilishi Mtakatifu wa Islam akatoka nao nje, na mbele za watu ambao yeye mwenyewe alikuwa amewaita; akatangaza akisema: Namtangaza Zaid kutokuwa tena mtumwa. sasa yeye yu mtu huru. Aidha natangaza kwamba nitamtendea kama mwanangu, na tokea sasa awe akijulikana kama Zaid bin Muhammad.

Sasa nitageukia upande mwingine wa utu wa Mtume Muhammad, kama bwana, kama baba na kama jamaa. Kuwahusu wanawake, yeye alitenda kwa wema na huruma hivi kwamba husikii ukali wowote toka kwake. Ingawaje zipo ripoti za Hadhrat Aisha r.a., na wakeze wengine kumkasirikia; yeye haripotiwi hata mara moja kuwa alipata kuwarukia kwa ukali kwa vyo vyote vile. Hadhrat Aisha r.a. anasimulia kwamba

alimsaidia kazi zake za nyumbani; haya yote yakiwa ni ziada ya wajibu wake kwa wanadamu wote kama Nabii wa Mungu. Akajishonea nguo zake; akajirekebishia viatu vyake; akajitekea maji na wala hakutaka msaada katika mambo haya. Upande huu wa tabia yake uliwapendeza sana masahaba zake. Baada ya kifo chake sahaba wake mmoja, alipokuwa akiendesha farasi, aliangusha mjeledi wake. Kijana mmoja akakimbia kwenda kumwokotea mjeledi wake lakini yeye kasema: Uache, tafadhali, hebu nishuke chini nikauokote mimi mwenyewe kwa sababu maisha yangu yote nimemuona Mwanzilishi Mtakatifu wa Islam hakutegemea wengine; hakumsumbua mtu mwingine kumfanyia kazi zake.

Tandiko lake laelezewa na Hadhrat Aisha, r.a. kuwa jifuko la ngozi lililojazwa majani. Anasema: Hakupata kula mkate wa ngano kwa siku tatu mfululizo. Zilikuwepo nyakati ambazo miezi iliweza kupita bila ya sisi kula nyama wala mkate, badala yake tuliyaruzuku matumbo yetu tende na maziwa, isipokuwa pengine zawadi isiyotazamiwa ambapo mtu angelichinja kondoo na kutuletea nyama. Hadhrat Umar r.a. anasimulia kwamba: Nilikwenda kwenye chumba kidogo alimokuwa akikaa Mwanzilishi Mtakatifu wa Islam. Alikuwa amelalia mkeka wa majani makavu uliokuwa mparuzi kiasi hiki kwamba ubavu uliolalia mkeka ule niliona ukijaa miparuzo. Nikakitupia jicho kile chumba na kilikuwa kitupu, hamkuwemo na chochote minghairi ya ndoo ya maji na kidubwana kimoja au viwili. Mimi nilimfahamu kuwa mpenzi mkubwa zaidi wa Mwenyezi Mungu, mja aliyekifikia kilele cha utu wema. Kulinganisha huku kukanihuzunisha kiasi hiki kwamba nikaanza kulia. Mtume Mtukufu akanigeukia na akasema: Umar waumwa na nini? Nikasema: Ewe Mtume wa Mungu, Mwenyezi Mungu, anakupenda sana; wewe ndiwe mbora wa alivyoviumba; lakini hata hivyo nakuona ukidhikika sana jinsi hii. Huna kitanda cha kufaa. Huna cho chote cha kupambia nyumba yako; hamna

cho chote. Mtume Mtukufu akatabasamu na akatamka akasema: Umar, je, wewe ungelipendelea vitu vya kidunia vya maisha haya kuliko vile tunavyowekewa na Mwenyezi Mungu katika maisha yajayo. Hadhrat Umar akajibu kwamba bila shaka vile vinavyokuja ndivyo bora zaidi, na mazungumzo yakakomea hapo.

Hiki kilikuwa kisa kidogo tu, lakini je, mzushi angeliweza kufanya hivyo? Kwa nini watu hutunga uwongo? Kwa minajili ya nini? Je, ni kwa ajili ya kuishi maisha ya dhiki na machungu kama hayo, na kwa ajili ya kushiriki katika shida za zama zao pamwe na watumishi wao waaminifu. Kama hayo ni kweli, basi ukweli wenyewe unakuwa hauna maana; kila kitu katika mwanadamu hapo kinakuwa bandia.

Yeye aliwahurumia hata wanyama. Siku moja alipokuwa safarini alimsikia ndege mdogo akitoa kelele za mahangaiko. Akawageukia masahaba zake na kuwauliza ni kitu gani kilichokuwa amefanyiwa ndege yule. Mmoja wao akajibu akisema kwamba alikuwa amempokonya mayai yake mawili. Mtume Mtukufu akasema: Yarudishe. Katika hadithi nyingine ya kisa hicho hicho yasemekana ni makinda wawili wala sio mayai yalikuwa yamechukuliwa, na Mtume Mtukufu akawaambia masahaba zake kwamba mama na asisononeshwe juu ya watoto wake. Hili halikuwa jambo la ndege na makinda, bali lilikuwa swala la utu wa watu maishani.

Mtume Mtukufu safari moja aliwasimulia masahaba zake kisa kimoja akisema: Mtu aliyekuwa na kiu jangwani, aligundua kisima kilichojaa maji. Akaingia kisimani na akanywa maji ya kumtosha. Alipotoka, akamwona mbwa akitweta kwa kiu; pengine alikaribia kufa. Yule mtu akarudi kisimani na akachota maji kwa viatu vyake, akavishikilia vizuri kwa meno yake akatoka kisimani, hapo akamnywesha maji yule mbwa.

Mwanzilishi Mtakatifu akaendelea kuelezea akisema: Mwenyezi Mungu ameniambia, mtu yule alisamehewa madhambi yake yote ya hapo kabla. Katika hadithi nyingine juu ya kisa hiki yasemekana ni mwanamke malaya aliyefanya hivyo. Maisha yake mazima yalijaa madhambi. Lakini akasamehewa mbele ya Mwenyezi Mungu kwa sababu ya kitendo cha kumhurumia mnyama.

Mmoja wa masahaba zake alimwuliza ya kwamba je, watapata thawabu kwa sababu ya vitendo vya kuwahurumia wanyama. Akasema: Naam, wanyama wale wote wenye maini chepechepe. Neno hili 'chepechepe katika Kiarabu hutumiwa kuonyesha wororo na uwezo wa kushtuka upesi. Mimi nimelitumia vile lilivyo lakini tafsiri yake ni ya mnyama ye yote ambaye kwa vyo vyote vile ni mwepesi wa kushtuka, awe akitendewa huruma, na Mwenyezi Mungu atalipa thawabu kwa vitendo vyote vya huruma namna hiyo.

Safari moja alimwona mtu akimkama mbuzi na akawa na wasiwasi wasije wanambuzi kutobakiziwa cho chote. Aliwakataza masahaba zake wasiuwe hivi hivi, ndege yeyote au mnyama. Akasema: Mtaulizwa na Mwenyezi Mungu juu ya kuua hivi hivi tu wala bila sababu nzuri. Alipoulizwa na ni sababu ipi inayoweza ikawa nzuri, alijibu akisema: Kama mnahitaji nyama, basi ueni. Kisha akawakumbusha ya kwamba hata katika kuua wasije wakakosa huruma: Ueni kwa njia ambayo kwayo mnyama atapata maumivu kidogo inavyowezekana. Baadhi ya Wanajumuiya wananiuliza kama ile njia ya kisasa ya kuua mnyama ni ya Kiislam; yaani kwanza kumziraisha mnyama na kisha kumchinja. Mimi nasema hiyo ndiyo hasa njia ya Kiislamu. Sikubaliani na wale wanachuoni wa Kiislamu, wanaosema kwamba njia hii haikufahamiwa na Islam ya hapo awali. Lakini vifaa hivi vinavyosaidia kuwapunguzia wanyama machungu havikuwa vikipatikana siku zile. Hili agizo ya kwamba hata

katika kuua onyesheni huruma, hata hivyo, lilitolewa na Mwanzilishi Mtakatifu wa Islam mwenyewe.

Sasa naligeukia lile swali la leo lenye kujadiliwa vikali; swala la kufuru. Kokote ninakotembelea ulimwengu, swali hili huniandama. Naulizwa ya kwamba je, wasemaje juu ya fatwa ya Khomeni ya kifo cha Salman Rushdie. Mimi huwaambia kwamba Islam niijuayo, niliyojifunza toka kwa Mwanzilishi Mtakatifu wa Islam, yatuambia kwamba hamna adhabu yoyote ile dhidi ya kufuru. Sio swala la kifo au kitu kinginecho. Miongoni mwa mambo mengine, mimi hukariri hususan kisa hiki kilichotokea maishani mwa Mtume Mtukufu; pia kimetajwa kwa ufupi ndani ya Qur'an Tukufu. Kabla ya kufika kwa Mtume Mtukufu huko Madina, mtu mmoja alikuwa akiinukia kwa maoni ya watu wote kuwa kama kiongozi wa makabila yote na makundi ya kidini. Alikuwa akiitwa Abdullah bin Ubayy bin Salul. Baada ya kuwasili Mtume Mtukufu mambo yakabadilika pole pole na badala yake yeye kwa kauli moja akakubaliwa awe kiongozi wa Madina. Japokuwa tofauti zilikuwepo, lakini kwa hakika, wake yeye ndio uliokuwa uongozi wenye mamlaka. Jambo hili likamfanya Abdullah bin Ubayy bin Salul awe mwivu kupindukia. Akawa yu mwenye kufichua moto wa sonono zake kwa njia hii au ile. Tabia yake ilikuwa ya aina ambayo kwayo Waislam wengine walimfahamu kuwa 'Mkuu wa Wanafiki'. Safari moja akiwa njiani toka vita ambavyo kwa jumla havikufaulu, na wapiganaji wote walikuwa wachovu sana tena walioudhika; mtu huyu Abdullah bin Ubayy bin Salul, akaona sasa ndio uliokuwa wakati wa kujilipizia kisasi. Miongoni mwa wenzake fulani yeye akatangaza akisema kwamba watakaporudi Madina, mheshimiwa miongoni mwao, atamfukuzilia mbali mnyonge zaidi miongoni mwao. Kauli hii ilikuwa wazi na kila mmoja alijua alichokimaanisha. Hadhrat Umar, r.a., baada ya kupata habari hii alimwomba Mtume Mtukufu ruhusa amuulie mbali mtu huyu; akasema kwamba Mtume Mtukufu karushiwa

matusi wasiyoweza kuyavumilia. Lakini Mtume Mtukufu hakuruhusu adhabu yoyote. Inaripotiwa kwamba mwanawe Abdullah bin Ubayy bin Salul, aliyeitwa Julabi Ubayy bin Salul, naye pia alifika mbele ya Mtume Mtukufu na akasema: Ewe Mtume wa Mungu, pengine kama ukimruhusu mtu mwingine amuue baba yangu, mimi nikiwa mwanawe, huenda nikawa na kinyongo. Baadaye katika wakati usiotazamiwa, huenda nikajaribu kujilipizia baba yangu na kumuua muuaji wake, na hivyo kutenda dhambi kubwa. Baba yangu anastahili adhabu hii kwa matusi aliyokutusi, kwa hivyo tafadhali niruhusu nimuulie mbali. Mtume Mtukufu akatabasamu na akasema: La, hasha, hapana adhabu. Wakarejea mjini Madina na kwa miaka mingi mtu huyu akaishi kwa amani chini ya ulinzi kamili wa Mwanzilishi Mtakatifu wa Islam, aliyekuwa amemtukana. Alipofariki, Mtume Mtukufu akaamua kusalisha sala yake ya jeneza. Hili halikuvumilika kwa baadhi ya masahaba zake. Hadhrat Umar r.a. anasimulia kwamba yeye alijaribu kumzuia na kasema: Si huyu ni mkubwa wa wanafiki. Huyu siye yule ambaye kumhusu yeye Mungu kasema kwamba hata kama ukimwombea msamaha mara sabini, hatasamehewa. Basi kwa nini, Ewe Mtume wa Mungu, uliye mpokeaji wa Wahyi huu wote, umeamua kusalisha sala yake ya jeneza. Jibu lilikuwa: Umar, simama kando. Ningelikuwa nayo matumaini kwamba Mwenyezi Mungu angelimsamehe kama nikimwombea zaidi ya mara sabini, mimi ningelifanya hivyo. Hiyo ndiyo iliyokuwa tabia ya Mwanzilishi Mtakatifu wa Islam. Alikuwa mtu mwenye huruma tele; mtu mwenye msimamo; mtu aliyeishi maisha ya ukweli na si kinginecho ila ukweli.

Alipoona kwamba siku za kurudi kwa Bwana wake Mtakatifu Allah zilikuwa zimewadia, aliwahutubia Waislam. Hii ilikuwa halaiki kubwa zaidi aliyopata kuihutubia. Hafla yenyewe ilikuwa Haji ya mwisho; inayojulikana pia kama Hijja-tul-Wida. Katika hotuba ile, ujumbe wake ulikwa kwa minajili ya wanadamu wote

na kwa wakati wote ujao. Aliwahutubia kama "Enyi wanadamu", hakusema Enyi Waislam lakini akasema: Enyi wanadamu, ninyi nyote mko sawa. Mwarabu si bora kuliko asiyekuwa Mwarabu, mtu mweupe si bora kuliko mweusi. Watu wote, wawe ni wa taifa au kabila gani, na wawe wanashikilia madaraka gani, wako sawa. Ubora wowote unaoweza kufikiriwa ni ucha-Mungu wa mtu. Mwishowe akasema: Hebu niambieni kama nimeufikisha ujumbe. Wote wakajibu kwa sauti moja wakisema: Naam, Ewe Mtume wa Mungu, kwa kweli ujumbe umeufikisha. Akasema: sasa nipeni ahadi kwamba mtazidi kuusambaza ujumbe huu kwa wanadamu wote, pembe zote za ulimwengu. Yeyote aliyepo hapa ni sharti aendelee kufikisha ujumbe huu kwa hao wasiokuwepo hapa na kazi hii ni sharti iendelee hadi mwisho wa ulimwengu.

Ubaguzi wa kitaifa ni swala linalojadiliwa vikali leo hii. Ingawaje mataifa mengi yaliyostaarabika yatakanusha kuwepo kwa jambo hili, uzoefu wangu baada ya kusafiri maeneo mengi, waonyesha kwamba ubaguzi huu wapatikana katika kila taifa na katika kila sehemu ya ulimwengu. Hili si tu swala la mweupe kujiona mbora kuliko mweusi, bali mweusi naye pia kujiona na ubora wa kuwa na nia ya kujilipizia kisasi dhidi ya weupe. Bado ndilo jambo la chini kwa chini lililo hatari zaidi katika fikara za kibinadamu na vihimizo. Chini ya maagizo bayana ya Mtume Mtukufu, mimi nawafikishieni ujumbe wa usawa wa wanadamu. Sisi sote tukiwa viumbe wa Mungu, tukiwa na chimbuko moja, twawezaje kujiruhusu kuporomoka kwenye kiwango ambapo tunatawaliwa na maswala ya ubora wa wanadamu kuliko wanadamu wengine.

Ulipokaribia wakati wake wa kuyatoka maisha haya, alihiyarishwa na Mwenyezi Mungu ama arudi kwake au apate ziada ya miaka katika maisha haya ya ardhini. Yeye jibu lake lilikuwa: Firifiqil Allah; Napendelea kurudi kwa Mola wangu Mtukufu. Haya pia ndiyo yaliyokuwa maneno yake ya mwisho

aliyotamka kabla ya kuingia maisha ya akhera.

Kama mnamwona kuwa yu mwongo basi bila shaka alikuwa nabii bandia. Kama si hivyo basi mimi ninaweza nikawahakikishieni kwamba hapana mtu mkweli awezaye akaambulia kuwa Nabii mwongo. Haiwezekani kabisa. Ni ufinyu wa fikara za mwanadamu unaovifanya vitu viwe tofauti na vile vilivyo. Ni mwanadamu ageuzaye ukweli kuwa uwongo na hekaya. Baadhi ya hekaya hubuniwa kwa mshabaha wa upendo; juhudi yenyewe ikimalizikia kutukuza daraja la mwanadamu hadi lile linalokiuka hilo, wakati mwingine hadi kufikia daraja la Mungu. Jambo hili limekuwa likitendeka katika dini zilizo nyingi zaidi ulimwenguni. Halikadhali tunaiona mandhari iliyo kinyume na hakika. Mtume Muhammad s.a.w. aligeuzwa kuwa hekaya ya chuki kwa karne nyingi na tabia hii isiyokubalika bado haijakoma. Tafadhalini mnapowahukumu watu, msiwahukumu katika misingi ya hekaya, wahukumuni juu ya misingi ya hali yao ilivyo kwa hakika.

Allah na awabarikini nyote na amani iwe juu yenu. Ahsanteni

**SEAL OF THE PROPHETS**
**Swahili Translation**

This book was first published as an address delivered by The Head of the Ahmadiyya Muslim Jamaat at Hounslaw London.
The address was shortly tries to clearup some misconceptions about the Holy Prophet's life.
On the other side the address tries to furnish the true picture of the Holy Prophet's life before and after his claim as the Prophet sent by Allah.
The address concludes to say that with all these good and noble characters of The Holy Founder of Islam it is impossible for him to be a False Prophet.